**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA MWANZA MHE. JOHN V.K. MONGELLA WAKATI UZINDUZI WA KAMPENI YA UGAWAJI WA DAWA ZA KUKINGA NA KUTIBU MAGONJWA YALIYOKUWA HAYAPEWI KIPAUMBELE KATIKA MKOA WA MWANZA TAREHE 18 JULAI, 2017**

Mhe. Hadijah Nyembo, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Ilemela,

Kamishina wa Polisi, Clodwig Mtweve, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza,

Dkt Leonard Subi, Mganga Mkuu wa Mkoa,

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya,

Viongozi mbalimbali waandamizi wa Serikali,

Wakuu wa idara za Sekeritarieti ya mkoa na wajumbe wa timu ya usimamizi wa shughuli za Afya (M) na wanahabari wote,

Mwalimu Mkuu na walimu wa Shule ya Msingi ya Isenga,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutulinda na kutuwezesha kukutana hapa leo na kushuhudia tukio hili muhimu la uzinduzi wa Kampeni ya umezeshaji wa dawa za Kukinga na Kutibu Ugonjwa wa Kichocho na Minyoo ya Tumbo

kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule, walioandikishwa na ambao hawajaandikishwa wenye umri wa kuanzia miaka mitano (5) hadi kumi na nne (14)

**Ndugu Washiriki,**

Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, hususani Kichocho na Minyoo ya tumbo yameathiri sehemu kubwa ya jamii katika Mkoa wetu wa Mwanza. Magonjwa haya huleta mahangaiko makubwa kwa wananchi hasa kwa watoto ikiwemo upungufu wa damu, kudhorotesha ukuaji, kupunguza mahudhurio ya watoto shuleni na pia kutofanya vizuri katika masomo yao. Ugonjwa wa Kichocho husababisha Saratani ya Kibofu cha mkojo ambayo haina tiba hadi sasa. Minyoo ya tumbo inaweza kusababisha Utumbo kuziba na mtu kulazimika kukatwa utumbo.

Magonjwa haya ni moja kati ya vyanzo vikuu vya umasikini katika familia, jamii, na taifa. Aidha, takwimu zimeonyesha kuwa wagonjwa walioathirika kwa saratani ya kibofu cha mkojo na haswa watokao kanda ya ziwa asilimia kubwa ya wagonjwa hao wengi wao chanzo chake ni maambukizi ya kichocho.

**Ndugu Washiriki,**

Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania iliridhia tamko la Shirika la Afya Duniani linalokusudia kudhibiti au kutokomeza magonjwa haya

ifikapo mwaka 2020, na ili kutekeleza azma hiyo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imetengeneza mpango kazi wa miaka mitano wa Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za udhibiti wa magonjwa haya.

**Ndugu Washiriki,**

Kitaifa, tafiti zilizofanyika mwaka 2005 zinaonyesha uwepo wa maambukizi ya kichocho yapo kati ya asilimia 12.7 hadi 87.6. Utafiti huo unaonyesha kwamba ugonjwa wa kichocho umeenea zaidi maeneo ya kando kando ya ziwa Viktoria na kiwango cha maambukizo ya kichocho ni zaidi ya 80% na kwa minyoo ya tumbo maambukizi ni 100% kwa baadhi ya maeneo.

Katika jamii za watoto wenye umri wa kwenda shule, tafiti kwa njia ya parasitologia, zimeonyesha uwepo wa ugonjwa huu ni zaidi ya 50%. Kwa kiwango hicho cha maambukizi, kwa mujibu wa tafiti na maelekezo ya kitaalam na Shirika la Afya Duniani (WHO), jamii inapaswa ipewe dawa za kukinga na kutibu. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za kitafiti za mwaka 2011 hadi 2015 kupitia taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu, NIMR Mwanza (SCORE Project), maambukizi ya magonjwa ya kichocho kwa Tanzania ni zaidi ya 51.5% ikiashiria kuwa yapata watu milioni 26 wameambukizwa. Utafiti huo umebaini kuwa takribani asilimia 50 ya watoto wenye umri wa kwenda shule yapata watoto milioni 6

wameambukizwa kichocho cha njia ya mkojo au kichocho cha tumbo au vyote.

**Ndugu Washiriki,**

Mkoa unawajulisha wananchi na wakazi wote wa mkoa wa Mwanza kuwa tarehe 18 Julai 2017 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele itaendesha kampeni ya Ugawaji wa dawa za Kukinga na Kutibu (Kinga – Tiba) kwa magonjwa ya Kichocho na Minyoo ya Tumbo. Walengwa wa kumeza dawa hizi ni watoto wote wenye umri wa kwenda shule ya msingi, miaka 5 – 14, walioandikishwa na ambao hawajaandikishwa.

**Ndugu Washiriki,**

Kampeni hii itaendeshwa na watalaam wa huduma za afya wakishirikiana na Walimu katika shule zote za msingi waliopatiwa mafunzo maalumu ya ugawaji wa dawa hizi. Kabla ya unywaji wa Dawa hizi Mtoto anatakiwa ale chakula na katika muda usiozidi masaa 2 baada ya kula awe amepatiwa dawa hizi; chakula kiandaliwe shuleni, na watoto wote wale chakula shuleni siku hiyo ya kumeza dawa.

Hivyo natoa wito kila mzazi katika Mkoa wa Mwanza anatakiwa amruhusu mtoto wake aende kumeza dawa hizi muhimu ili ajikinge na

kupata tiba ya magonjwa haya hatari kwani huduma hii ya dawa za kinga tiba inatolewa bila malipo kwa kila mtoto.

**Ndugu Washiriki,**

Dawa hizi zimethibitishwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuwa ni salama, hazina madhara kwa afya ya binadamu zinapomezwa kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wahudumu wa Aafya na Walimu waliopewa mafunzo.

Dawa zitakazohusika ni za **Praziquantel** za udhibiti wa Kichocho na **Albendazole** za udhibiti wa Minyoo ya tumbo ambazo zitatolewa kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule, walioandikishwa na ambao hawakuandikishwa.

**Ndugu Washiriki,**

Ni matumaini ya Mkoa na Halmashauri zake kuwa Wazazi mtawaruhusu watoto wajitokeza kwa wingi kumeza dawa hizi, kwa Ustawi wa Afya ya Jamii ya mkoa wetu wa Mwanza.

Sasa nipo tayari kuzindua kampeni ya Ugawaji wa Dawa za Kukinga na kutibu Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele katika Mkoa wa Mwanza.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**